BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Pili – Tarehe 13 Februari, 2025.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

80. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, visiwa vya Zanzibar vimeathirika na huenda vikaathirika zaidi kutokana na hali hiyo.

    Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na changamoto hiyo.

**Ofisi ya Rais Ikulu:**

118. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu:

    Kwa kiasi gani Serikali inapambana na suala zima la udukuzi kupitia mifumo yake mbali mbali inayoanzishwa ili kuweza kuwa na uhakika wa usalama wa mifumo hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

135. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Kwa sasa kuna watoa huduma wangapi kwa maana ya kampuni na vikundi vilivyopatiwa zabuni ya usafi katika taasisi za Serikali na kwa kiasi gani vinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa mikataba walioingia na taasisi hizo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

62. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa hatua ilizozifikia za kuwataka wananchi kuyasajili maeneo yao ya

ardhi wanayoyamiliki kwa lengo la kupunguza migogoro nchini.

(a) Ni hatua zipi wananchi wanapaswa kuzifuata wanapotaka kusajili maeneo yao.

(b) Ni zipi gharama halisi za usajili huo ambazo zimewekwa na Serikali kisheria.

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:</u>**

153. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ili jamii iwe na ustawi bora inahitaji afya njema ya kimwili na kiakili kumrahisishia mtu kufanya kazi zake akiwa na utimamu.

(a) Je, tathmini iko vipi juu ya idadi ya wataalamu wa ustawi wa jamii.

(b) Kwa kiasi gani maofisa wa ustawi wa jamii wanajengwa kuwa na uelewa wa kujua mambo katika jamii zao katika kueneza elimu ya ustawi wa jamii kwa ufanisi.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

5. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mualiko wa Mufti Menk hapa nchini kwetu jambo ambalo limeifanya Zanzibar kuonekana na kujulikana katika mataifa mbali mbali duniani.

Je, Wizara ina mpango gani wa hapo baadae kuwapa kadi maalum za mialiko watu kama hawa maarufu duniani, ikiwa ni moja ya mikakati ya kuitangaza nchi yetu duniani kote.

19. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Waongozaji Watalii “Tour Guides” ni watu muhimu sana wanaotoa taswira halisi ya nchi yetu.

Ni taratibu gani zinazotumika katika kuwaongezea ujuzi na elimu ya kazi yao ili waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi na kwa viwango vya kimataifa.

<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

29. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kilimo chetu kwa umuhimu wake kimepitia katika kauli mbiu mbali mbali zikiwemo Kilimo Kwanza, Siasa ni Kilimo, Kilimo ni Uti wa Mgongo na nyenginezo.

(a) Je, kwa sasa ni ipi kaulimbiu ya kimkakati ya kusukuma maendeleo ya sekta ya kilimo.

(b) Je, kwa kiasi gani kaulimbiu hii inayasadifu malengo yake.

31. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mpaka sasa ni aina gani ya mbegu bora zilizoibuliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo - ZARI.

<u>Wizara ya Afya:</u>

65. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua ilizozichukuwa za kujenga hospitali katika kila Wilaya kwa lengo la kuimarisha huduma za afya nchini.

(a) Katika Hospitali ya Lumumba kumejitokeza changamoto ya mlundikano wa wananchi wanaofika kuangalia wagonjwa hospitalini hapo. Je, ni zipi hasa sababu zinazopelekea mlundikano huo.

(b) Ni upi utaratibu hasa wa kuangalia wagonjwa kwa wananchi wanaofika hospitalini hapo.

103. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna taarifa kuwa tatizo la minyoo limekuwa likigharimu maisha ya watu siku hadi siku pamoja na jitihada za Serikali za kupambana na tatizo hilo.

Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya tuhuma hizo.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

97. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni kwa kiasi gani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inafikiria kuwekeza kwenye “Public Private Partnership” (PPP) kupitia mfumo mpya wa mitaala wa kupima umahiri.

98. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Kwa sasa ni skuli ngapi zimeanza kutoa mafunzo ya amali kwa muktadha wa mabadiliko ya mtaala mpya.

(b) Nini matarajio ya ongezeko la shule kama hizi kwa mwakani.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

1. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Kumekuwepo na mabadiliko ya nauli za boti na meli zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam, Unguja na Pemba mara kwa mara bila ya wananchi kupatiwa taarifa za kutosha. Jambo hili limekuwa likileta malalamiko makubwa na usumbufu kwa wananchi wanaotumia usafiri huo.

   (a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha mabadiliko ya bei ya nauli za boti mara kwa mara.

   (b) Je, ni muongozo gani wa kisheria huhitajika katika kubadilisha nauli za boti na meli zinazofanya safari hapa nchini.

   (c) Je, ni namna gani Serikali inawashirikisha wananchi katika mabadiliko haya ya nauli za usafiri wa baharini.

107. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

   Ni kwa kiasi gani ujenzi wa miundombinu ya barabara “flyover”, madaraja na vivuko mbali mbali utasaidia katika kupambana na umaskini Zanzibar.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

101. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

   Kitathmini kila Mzanzibari anakula kilo ngapi za samaki kwa mwaka kwa muktadha wa kunufaika na rasilimali ya mzunguko wa bahari tulionao.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
13 Februari, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.